

COMPANY HIGHLIGHT

# Programu ya Utafiti KVTC

na Andrew Callister, PhD

## Tafiti ya Sayansi ya Misitu; Ni nini na kwa nini ni muhimu?

Tafiti ya matumizi ya sayansi ya misitu inahusisha majaribio ya eneo husika kutambua utaratibu mzuri wa usimamizi na malighafi za kimaumbile kwa malengo ya biashara. Programu ya utafiti inaelekezwa zaidi na mahitaji na fursa ya kila kampuni.

## Tafiti za KVTC kabla ya 2013

KVTC mapema ilitekeleza taratibu za kiubunifu kama vile kutumia mbegu bora (clones) na matumizi ya mbolea kwenye maeneo yasiyo na rutuba. Majaribio ya maumbile/jene KVTC yalianza siku za nyuma 2004.

## Tafiti 2013 na Kuendelea

Nilianza kufanya kazi na KVTC 2013 ili kuongeza nguvu kwenye programu yake ya tafiti na kuongeza mafanikio ya shughuli maboresho ya maumbile, ukuzaji mbolea, na upunguziaji sawia. 2013 tulianzisha mradi wa PROJECT PLUS 20, programu ya miaka kumi ikiwa na lengo la kuongeza mapato kwa kutumia mbegu bora (clones) na kuendeleza taratibu nzuri maalumu za ukuzaji miti kulingana na eneo husika.

Katika miaka mitano ya mwanzo, PROJECT PLUS 20 imefanikiwa kufanya majaribio shambani ya jamii 190 na viploti (clones) 880 katika maeneo saba ikiwakilisha ufanisi mpana wa kimazingira. PROJECT PLUS 20 inalenga kuboresha jamii ya mitiki inayopatikana Tanzania, ambayo imethibitishwa kufanya vizuri katika mazingira ya ukuzi KVTC dhidi ya mchanganyiko wa maumbile/jene kutoka vyanzo vingine.

Majaribio ya Mwitiko wa Mbolea umethibitisha kiwango kukubwa cha manufaa kitapatikana kwa kutia mbolea shambani baada ya punguzo la kwanza. Utekelezaji wa kibiashara wa kukuza mbolea baada ya kupunguzia unatarajia kuongeza ukuaji wa wastani 40% kutegemeana na daraja la eneo husika.

Matokeo ya tafiti yameunga mkono jitihada za KVTC 2012/13 kwa kuweka mpango wa upunguziaji kutokana na tofauti ya ukuaji wa mashamba binafsi.

## Mtazamo wa Mbele

Hatua inayofuata PROJECT PLUS 20 ni kutambua viploti (elite clones) vizuri vya majaribio ya maumbile/jene kwa uzalishaji wa kibiashara. Majaribio yanayo endelea ya Mwitiko ukuzaji mbolea na upunguziaji miti utasidia kuunda muundo unao endana na ukuaji, ambao utasaidia kuboresha maamuzi ya kiusimamizi na ukadiriaji wa mavuno. Kwa taarifa zaidi wasiliana na: andrew@treehouseconsulting.com.au

HIGHLIGHTS



## #NZS2018 Mbio za Baiskeli

KVTC ilifadhiri mashindano ya baiskeli ya mwaka 2018 North Zanzibar Sportive. Zanzibar ni soko muhimu kwa KVTC na mbio zilitoa fursa kuonyesha upande tofauti wa kampuni katika soko muhimu la ndani.

Tunatarajia kuonana mwakani katika **#NZS2019**!!



## Semina ya Wakulima wa nje

Oktoba 30, KVTC itawaleta pamoja karibu wakulima wadogo 500 kwenye semina kujifunza zaidi kuhusu mtazamo wa mbele na fursa ukuzaji mitiki katika bonde la Kilombero. Taasisi za mitaji midogo na benki wanatarajia kushiriki kwenye semina hii. Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na semina timu OSP team.

# Kutoka Dawati la Hans

na Hans Lemm

Tuko katikati ya msimu wa moto na joto linapanda katika bonde la kilombero ingawa maeneo ya pwani yanaendelea kupata mvua. Wafanyakazi wetu wanafanya jitihada kudhibiti tishio la moto. Tunawatu mashambani usiku na mchana wakifanya doria na minara ya moto ina watu mda wote. **Tafadhari tusaidie sisi kudhibiti moto!!**

Msimu wa kiangazi ni wakati tunajishughulisha zaidi kununua magogo kutoka kwa wakulima wadogo na tunarajia manunuzi kuwa mara mbili zaidi ukilinganisha na ya mwaka jana. Makala muhimu katika awamu hii inahusu tafiti ya elimu ya misitu tumizi.

(Makala muhimu katika awamu hii inahusu tafiti ya elimu ya misitu tumizi inayofanyika KVTC. Ni wakati wa kutabasamu sana tukiwa katikati ya miaka 10 ya program iliyoanza 2013. Tayari sasa tunaweza kuanza kupima mafanikio yaliyopatikana na kubadili tafiti kuwa sehemu shughuli bora kabisa za utendaji.

Mwezi huu wa kumi tunaenda kuwaleta pamoja wakulima wote wa nje pamoja katika semina ya kwanza kabisa katika programu ya kuwawezesha wakulima wa nje (OSP). Jumla ya wakulima 500 watakutana Ifakara kushirikishwa uzoefu na kubadilishana mawazo na wafanyakazi wa kampuni lakini pia na wawakilishi wa Programu ya Misitu kwa Watu binafsi na taasisi kadhaa za fedha.

Mwisho napenda kuangazia jitihada za timu ya waendesha baiskeli KVTC katika #NZS2018. Timu ilionekana vizuri na kati yao watatu walishika nafasi kati ya 10 bora na matokeo timu ya KVTC walipata zawadi ya jumla ya timu.





*One more picture of a Team KVTC rider from the #NZS2018.*

## UPDATE KVTC BIOMASS CHALLENGE

Septemba 6 KVTC ilisaini mkataba na kiwanda cha Ujerumani kinachoitwa Sustainable Charcoal Cycle Industries. SCCI itawekeza kwenye kiwanda kipya kitakacho jengwa karibu na kiwanda cha KVTC

## JE UNAJUA?

Mtiki ni moja ya jamii ya Mint. Watu wa asili huko inakopatikana kwa wingi, kama Myanmar, walitumia kutengeneza chai kutokana na magamba ya mti wa mtiki.

## TUSIKILIZE

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

# Maeneo ya Miti ya Asili

na Kennedy Haule & Hans Lemm

## Muda wa Historia

KVTC ilianza 1992 hata hivyo mawazo ya KVTC yalianza nyuma miaka ya 80's wakati huo serikali ya Tanzania na muwekezaji kiongozi, Shirika la maendeleo la Jumuiya ya madola walijadiliana kuhusu mradi. Kufuatia hilo CDC ilianzisha tafiti kadhaa juu ya uwezekano wa mradi zikiwemo za tathmini ya athari ya mazingira iliyofanywa na taasisi tathmini ya raslimali ya Chuo Kikuu Dar Es Salaam na taasisi ya kimataifaya Mazingira na Maendeleo ya Uingereza. kati ya mapendekezo mengi moja muhimu ni kujumuisha kiwango kikubwa cha misitu ya miombo katika shamba kubwa wakati mitiki ikikuzwa kwenye vishamba vikizungukwa na misitu ya asili "mosaic" na KVTC ikisimamia hii ardhi ya miombo kwa urendelevu.

## Eneo la Udhibiti wa Wanyama Kilombero na Uunganishaji

Kwa miaka, misitu ya KVTC imekuwa sehemu uunganishaji na ushoruba inayounganisha Hifadhi ya pori ya Selous na Milima ya Udzungwa. Misitu ya KVTC vilevile ni sehemu ya mfumo wa maji unaorisha mto Kilombero na baadae mto Rufiji hadi delta yake na matokeo bonde la Kilombero linapokea ongezeko la umakini kutoka kwa watendaji katika maswala ya hifadhi.

Bonde limetatambuliwa kuwa ni Eneo la Ramsar na linachangia maji kwa zaidi 50% katika mradi mkubwa wa bwawa la umeme uliopangwa kujengwa

## Maendeleo ya Mbele

Wakati Uongozi wa KVTC umejidhatiti kutunza misitu ya asili katika khali nzuri, tunagundua kuongezeka kwa msukumo katika raslimali adimu, inawezekana tunahitaji kuangalia upya muundo wa usimamizi.

Tunaangalia karibu na wadau kadhaa katika kutafuta muundo mpya na njia bunifu ya kulinda thamani ya mazingira kwa misitu yetu wakati tukiongeza manufaa ya kiuchumi kwa jamii inayotuzunguka.

## WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE : kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ